STANDARD EIGHT MID-TERM 3 EXAMS

2016

KISWAHILI PAPER

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com |
Website:www.schoolsnetkenya.com

NATIONAL SERIES 2016 KISWAHILI

Muda: Saa 1 Dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu kina maswali 50.

2. Ukiwa utataka kuandikia chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.

3. Ukisha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU,** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.

5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu.

NAMBARI YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule. Na namba za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.

7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.

8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.

9. Kwa kila swali 1 - 5 umepewa majibu manne. Majib u hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi ilionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano:

27. Chagua sentensi yenye istiara.
A. Bwana Abeti ni kamusi
B. Kidosho yule amefungasha
C. Ameangusha gunia la viazi
D. Moyo wake ulimhadaa
Jibu ni A.

24. [A] [B] [C] [D] **25.** [A] [B] [C] [D] **26.** [A] [B] [C] [D] **27.** ~~[A]~~ [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **20,** kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.

12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Mwanafunzi aangalie ya kuwa maswali yote kwenye Kitabu yamepigwa chapa.

FUNGUA KURASA

Jaza viasho 1 -15 kwa maneno mwafaka.

Elimu ni ___ 1 _____ la tajriba mbalimbali, ____ 2 ___ kila _____ 3 _____ tunajifunza, kila nukta ___ 4 _____ ya maisha yetu huwa ni mwanzo wa ____ 5 ____ ____ 6 ____ inayomulika na ____ 7 _____ siku ya usoni. Kila leo ____ 8 _____ kesho ____ 9 _____ na hali kadhalika.

	A	B	C	D
1.	matukio	tukia	tukio	tukika
2.	la	na	cha	wa
3.	tunapumua	tunafumua	tunapotumwa	tunapopumwa'
4.	kipya	mpya	jipya	wapya
5.	tajiri	jaribu	tajriba	jaribu
6.	ngeni	mgeni	geni	kigeni
7.	kulekeza	kuelezwa	kuelekezwa	kuelekezeka
8.	inaathiriwa	inaathiri	athirika	athiri
9.	wake	yake	chake	lake

____ 10 ____ wa vijana wale aliniamuru niingie ndani, ____ 11 _____ na baridi humo. Nilitetemeka ____ 12 ____ nikazidi kuuma meno ____ 13 ____ lisilo budi hubidi. Alinikabidhi matunda mbalimbali kama vile zabibu na parachichi ili _____ 14 _____. Nilimshukuru na nikaelewa _____ 15 _____

10.	mojawapo	mmojawapo	kimojawapo	moja
11.	kulikuwa	ilikuwa	mlikuwa	palikuwa
12.	bali	mbali	japo	aidha
13.	iwapo	ikiwa	kamavile	mithili
14.	nilishtaki njaa	nikastaki njaa	nashtaki njaa	kushtaki njaa

15. A. Mgala muue lakini haki mpe.

B. Mla nawe hafi nawe.

C. Ibilisi wa mtu ni mtu.

D. Ajizi ni nyumba ya njaa.

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

Jibu maswali 16 - 30 kulingana na maagizo.

16. Tuliandaliwa wali **kwa** nyama ya kasa : kwa ilivyotumiwa inaleta dhana ya
    A. kimilikishi
    B. namna
    C. kitumizi
    D. pamoja
17. Marashi _____ _____ niliyotumwa kununua kutoka mjini
    A. haya ndiyo
    B. hii ndio
    C. haya ndio
    D. hizi ndiyo
18. Ni ipi isiyokuwa nomino katika ngeli ya I - ZI
    A. Nguo
    B. Kalamu
    C. Dawati
    D. Tarakilishi
19. Chagua neno ambalo lina silabi ambatano
    A. mmeng'enyo
    B. cherehani
    C. chungwa
    D. jembe
20. Kamilisha: mashabiki walifurika uwanjani ___
    A. marshimarshi
    B. chekwa chekwa
    C. mzozo
    D. furifuri
21. Onyesha jina lisilofaa katika orodha ifuatayo
    A. kaputula
    B. kichocho
    C. tetewanga
    D. kichusi
22. Ugonjwa wa kiseyeye huathiri sehemu zipi za mwili
    A. ngozi
    B. fizi
    C. mapafu
    D. tumbo
23. Mtimkuu aliwauliza wanawe ikiwa wangeenda ukumbini alasiri ya siku hiyo: Sentensi hii katika kauli halisi itakuwa:
    A. " Mtaenda ukumbuni leo alasiri?" Mtimkuu aliwauliza wanawe.
    B. "Mgeenda ukumbuni leo alasiri ?" Mtimkuu aliwauliza wanawe.
    C. Mtaenda ukumbuni leo alasiri? " Mtimkuu aliwauliza wanawe."
    D. "Mngelienda ukumbuni leo alasiri?" "Mtimkuu aliwauza wanawe?".
24. Ni sentensi ipi iliyo sahihi kisarufi?
    A. Cherehani ambayo iliharibika ni yake
    B. Cherehani ambacho kiliharibika ni chake
    C. Cherehani ilioharibika ni yake.
    D. cherehani iliyoharibika ni chake
25. Fuma ni kusuka nyuzi . Vile vile fuma ni ___
    A. kudung a kwa kifaa chenye makali
    B. kudunga kwa mtutu wa bunduki.
    C. kishona nguo paliporaruka.
    D. kupachika nguo kiraka kipya.
26. Ni sentensi ipi ina matumizi ya _ "ki" ya wakati?
    A. Akija nitafurahi.
    B. Kijitu hiki ni kibaya.
    C. Alipoenda kwake alimkuta akilala.
    D. Alifanya kiungwana kumpelekea pesa zake
27. Chagua orodha ya vitenzi pekee
    A. uza, oza, chapa, changa
    B. sana, vyema, bivu, laini
    C. mengi, safi, uchu, rangi
    D. hicho, hii, vile, haya
28. Ipi si sahihi?
    A. Bumba la nyuki
    B. Buda la noti
    C. Kigaro cha askari
    D. kaumu ya watu.

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

29. Hawa ni wageni hawa si wenyeji.
Ni sawa kusema
A. hawa si wenyeji bali ni wageni.
B. hawa si wageni bali ni wenyeji.
C. hawa si wageni wala si wenyeji.
D. hawa ni wenyeji si wageni.

30. Andika wingi wa wastani wa sentensi ifuatayo: kilango kinanivutia
A. vilango vinanivutia.
B. mlango unanivutia.
C. milango inatuvutia.
D. milango inanivutia.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31- 40.

Kijiji cha mashaka kilikuwa katika mji wa matatizo. Kijiji hiki kilikumbwa na shida nyingi mno. Mbali na kuwa nchi ilikuwa na udongo wenye rotuba, kijiji hiki kilitegemea vijiji jirani ili kupata chakula. Hali hii ilibaki kuwa ya kusikitisha sana. Viongozi wake walikuwa watu wenye mate ya fisi wala hawakujali hata kidogo maisha ya wananchi wake. Kwao uongozi ulikuwa nafasi mwafaka ya kujitajirisha kwa kujilimbikizia mali na kufaidi jamaa zao.

Hatimaye raia wake walichoka na ikawalazimu kuchukua hatua mbadala. Walisema wazee kuwa lisilo budi hubidi. Wananchi walifanya mkutano wa dharura na kuelezana matatizo yao. Baadhi ya kuwaza na kuwazua , uamuzi ulifikiwa kuwa ni lazima kufanywa uchaguzi wa dharura ili kuyaokoa maisha ya wanakijiji.

Wakati wa kupendekeza majina, kijana Hekima aliomba fursa ya kusema machache kwa niaba ya vijana. Kwa kuwa palipo na wazee hapaharibiki neno, waze waliona ni jambo la busara kupata maoni ya vijana kwani nao pia walikuwa na haki zao za kutetea.

Kijana alipoinuka aliwaamkia wazee kwa taadhima kuu na kuwateka mahudhura bakunja. Kisha akasema, "Naomba samahani kwa kusema mbele za wazee watukuka. Ni moyo ulionisukuma nami nikawa sina uwezo wa kujizuia. Naomba kwa aibu zote kusema kuwa kiongozi atakayetufaa sisi wana mashaka ni lazima aweze kutekeleza yafuatayo kwanza, awe mnyenyekevu, asiyekuwa na kiburi wala tamaa ya mali. Pili, awe na uwezo wa kuwaunganisha wanakijiji wote ili tuwe jamii moja isiyoangalia misingi ya lugha zetu ama mila yetu na kinyume chake. Atuweke pamoja na kutuongoza kuzungumza lugha moja- mwisho, wazee wangu, kiongozi huyu ana wajibu wa kuwa na mlango na sikio wazi kwa wote bila kujali kuwa huyu anatoka katika ukoo wake au la . Nawashukuru nyote kwa kunipa fursa nawatakia kila la heri na fanaka kwa kijiji cha Mashaka".

Baada ya kauli ya kijana yule, wote waliokuwapo walikubaliana kwa kauli moja kuwa mzee Maarifa alitosha kuwa kiongozi wao na akachaguliwa bila kupingwa .Wananchi wote walikuwa tayari kumwunga mkono na kuendeleza nchi. Mzee Maarifa alikuwa mwadilifu aliyeteua kamati sita muhimu na kuzipa maagizo maalum. Kamati zilizoshirikiana na kuleta mabadiliko na kukifanya Mashaka kuwa kijiji kilichopigiwa mfano ni: Kamati ya mazingira , kamati ya elimu, kamati ya uchumi na uwekezaji, kamati ya kilimo na chakula , kamati ya maadili na desturi na kamati ya usalama.

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

31. Katika aya ya kwanza, mwandishi anasema kuwa
A. kijiji hiki kiliwalisha majirani zake mbali na kuwa na matatizo mengi.
B. Wanakijiji hiki hawakuweza kulima licha ya kuwa na mashamba yenye rotuba.
C. wanakijiji hawa waliweza kulima licha ya kuwa na mashamba yasiyo na rotuba
D. kijiji hiki kilikuwa katikati ya nchi iliyokuwa na udongo usiokuwa na rotuba.

32. Kifungu watu wenye mate ya fisi kimetumiwa kwa maana ya _____
A. viongozi wenye tamaa.
B. viongozi walevi kupindukia.
C. viongozi wangwana.
D. viongozi waadilifu na wahisani.

33. Katika aya ya kwanza, mwandishi ana maoni yapi kuhusu viongozi katika kijiji hiki?
A. Ni watu wanaojali maslahi ya raia kwa mapana.
B. Ni watu wenye ubinafsi mkubwa.
C. Ni watu waadilifu wenye utu na uungwana.
D. Ni watu wasiokuwa na upendeleo wowote.

34. Katika aya ya pili, ni nahau gani inayojitokeza na kuwasukuma wanakijiji hawa?
A. Kufika njia panda.
B. Mambo kuwafika kooni.
C. Kupasua mbarika
D. Kulia ngoa.

35. Picha inayojitokeza katika aya ya tatu kuhusu msimamo wa wazee ni kwamba
A. vijana walikuwa na mamlaka mbele ya wazee.
B. wazee waliwagandamiza vijana
C. wazee hawakuwa na busara ya uamuzi
D. vijana hawakuruhusiwa kusema mbele ya wazee

36. Vijana walipewa fursa kueleza mawazo yao kwa misingi ya kuwa na _____
A. haki ya kujitetea
B. haki za kutetea
C. haki ya kuteta
D. haki ya kuteseka.

37. Unafikiri ni kwa nini kijana huyu aliwateka mahudhura bakunja?
A. kwa ulumbi wake
B. kwa malumbano yake
C. kwa ubishi wake.
D. kwa uzushi wake.

38. Katika kutaja sifa bainifu za kiongozi aliyewafaa raia, kijana alitaja sifa ngapi?
A. Aroba
B. Matano
C. Tandatu
D. Matatu

39. Kutokana na ufanisi wa kijiji cha mashaka chini ya bwana maarifa, tunaweza kusema kuwa _____
A. kofi hulia kwa kiganja kimoja.
B. mkono mmoja huweza kumchinja ng'ombe.
C. ni vigumu kidole kimoja kumvunja chawa.
D. nia nyingi hazichimbi shimo.

40. Kifungu hiki kinadekuza ujumbe upi muhimu kwetu katika jamii
A. viongozi wabadhirifu wana uwezo mkubwa wa kuijenga nchi.
B. viongozi waadilifu kuweza kuleta ufanisi katika jamii
C. viongozi mafisadi wana mbinu mbadala wa kuijenga nchi.
D. vijana watundu huwasaidia wazee kubuni mikakati bora ya ujenzi.

Soma kifungu kisha ujibu maswali 41- 50.

Binadamu duniani amezungukwa na vitu vinavyoitwa maliasili, yaani ; ardhi, maji, hewa , wanyama, mimea , madini na kadhalika ambavyo ndivyo vilivyo uti wa mgongo wa maisha.

Katika mipango ya nchi yoyote huwa kuna wizara moja zaidi ambayo hukabidhiwa jukumu na wajibu wa kuhifadhi mali haya asili ili yaweze kumsaidia binadamu kuyaendeleza maisha yake. Na papo hapo kuhakikisha yanabaki bila kuhabiribiwa kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Ili binadamu aweze na kumudu kuyatumia mali haya ya asili kwa busara na hekima, anawajibika kuyaelewa maliasili yenyewe, mazingira yake, maisha yake, maana yake na umuhimu

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

wake mithili, ya viungo vya maisha. Mtu asiyeyaelewa mambo haya mathalani, anaweza kuifyeka misitu kwa tamaa ya kupata shamba kubwa zaidi la kupandia mahindi. Lakini hatimaye asilipate walau hindi moja kwa sababu ya ukosefu wa mvua utakaoletwa na ukame wa kuondoka kwa miti.

Katika nchi yetu ipo wizara ya maliasili ambayo imekabidhiwa jukumu la kulinda, kutunza na kuhifadhi maliasili haya. Bahati mbaya, elimu . Nyingi za mambo ya maliasili zimeandikwa katika vitabu kwa lugha ya ung'eng'e. Kwa hiyo, elimu hizo ni adimu kuwafikia wazalendo walio wengi. Licha ya hayo, mimi na wewe tufanye juu chini kuwaelimisha wenzetu kuhusu maliasili na umuhimu wa kuyahifadhi mazingira yetu kwa jumla.

41. Chagua kauli sahihi zaidi
    A. binadamu amezingirwa na maliasili.
    B. binadamu amezungukwa na mali mengi maishani.
    C. mazingira yamezungushwa na maliasili
    D. uti wa mgongo ni maliasili katika mazingira.
42. Katika aya ya kwanza, tunadokezwa kwamba _____
    A. binadamu ana uti wa mgongo wa maisha
    B. vitu vinavyoitwa mazingira ni maliasili
    C. binadamu ndiye chanzo cha maliasili
    D. maliasili yana umuhimu mkuu katika maisha.
43. Aya ya pili inataja kwamba _____
    A. wizara husimamia maliasili na mazingira'
    B. mazingira na wizara huwajibikia maliasili
    C. kuna mipango ya binadamu kuendeza wizara ya maliasili
    D. wizara husaidia vizazi vijavyo visiharibu mazingira.
44. Binadamu anaweza tu kuyatumia maliasili vizuri _____
    A. akiyaelewa na kuyathamini.
    B. akitumia busara na hekima kwa kilimo
    C. akiwa na viungo vyake maishani
    D. asipofyeka misitu
45. Tunaambiwa kwamba anayewania kuifyeka misitu ili apate shamba kubwa alimie mahindi, huenda asivune hata hindi moja kwani _____
    A. mahindi hayastawi porini.
    B. misitu huharibu mahindi.
    C. misitu ndiyo huvuta mvua ambavyo ingemstawishia mahindi.
    D. kufyeka mahindi ni kuharibu maliasili.
46. Taarifa inasema . Kazi kuu ya wizara ya maliasili _____
    A. ni kuleta mvua na ustawi wa misitu.
    B. ni kukabidhi jukumu kwa wananchi.
    C. ni kuandika vitabu kwa kimombo.
    D. kuhifadhi mazingira, maliasili ya watu wake.
47. Katika sarufi ya lugha ya kiswahili neno **maliasili** ni
    A. kisawe.
    B. tashbihi.
    C. nomino ambata.
    D. msamiati.
48. Katika taarifa, mwandishi anasema, "Lakini hatimaye asilipate "walau" hindi moja ....." Neno walau limetumika kwa maana si sawa na lipi ya haya?
    A. japo
    B. ingawa
    C. ila
    D. falau
49. Mimi na wewe tunashauriwa tufanye nini katika kutekeleza wajibu na kuhifadhi mazingira na maliasili?
    A. Tutafsiri vitabu vya ung'eng'e katika kiswahili.
    B. Tuwasaidie wananchi wenye elimu adimu.
    C. Tuwafafanulie wananchi sera mahsusi za kudhibiti uharibifu wa mazingira na maliasili.
    D. Tuwe walimu na wazalendo.
50. Kichwa kinachofaa zaidi habari hii ni
    A. Wizara ya maliasili na mazingira.
    B. Umuhimu wa kuhifadhi maliasili na mazingira.
    C. Binadamu na mazingira.
    D. Mazingira na maliasili.

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27